**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA**
**KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA TATU (JANUARI – MACHI, 2024) ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA LEWIS KALINJUNA TAREHE 29 - 30.04 .2024**

## A. WAJUMBE

**WALIOHUDHURIA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Elias R. Masumbuko | Mstahiki Meya (Mwenyekiti) |
| 2. | Mwl. Mary Maka | Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa (Katibu) |
| 3. | Mhe. Zamda S. Mwebea | Naibu Meya |
| 4. | Mhe. James M. Matinde | Mjumbe |
| 5. | Mhe. John P. Kisandu | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Picca N. Chogero | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Sheilla D. Mshandete | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Victor T. Mmanywa | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Moshi H. Kanji | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Hassan R. Mwendapole | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Msabila M. Kulwa | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Zuhura Waziri | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Juma M. Nkwabi | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Reuben N. Kitinya | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Mussa E. Andrea | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Mariam L. Nyangaka | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Paschazia C. Seni | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Peter J. Kwoliba | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Victor Y. Mkwizu | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Esther F. Makune | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Ezekiel J Sabo | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Reuben M. Dotto | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Gulamhafeez Mukadam | Mjumbe |

## B. WASIOHUDHURIA

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Patrobas Katambi (MB) | Kwa taarifa |
| 2. | Mhe. Lucy Mayenga (Mbunge VM) | Kwa taarifa |
| 3. | Mhe. Enock Lyeta | Kwa taarifa |

**C. WATAALAM**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Pius M. Sayayi | Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu. |
| 2. | Kuchibanda K. Snatus | Mkuu wa Kitengo cha usimamizi wa Taka na Usafi wa Mazingira. |
| 3. | Charles Luchagula | Mkuu wa Kitengo cha Utamaduni, Michezo na Vijana |
| 4. | Jesca Kipingu | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini. |
| 5. | Mensaria Mrema | Mkuu wa Divisheni ya Mipango na uratibu |
| 6. | Naely Elias | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji |
| 7. | Lenard Chepe | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA. |
| 8. | Eng Boaz Kayira | Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu, maendeleo ya Vijiji na Miji. |
| 9. | Peter Chuwa | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. |
| 10. | John Tesha | Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii. |
| 11. | Ezra Manjerenga | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhifadhi wa Maliasili na Mazingira. |
| 12. | Mary S. Maka | Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi |
| 13. | Lucas Mzungu | Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari. |
| 14. | Octavina Kiwone | Mratibu TASAF |
| 15. | Jacob Mwinuka | Afisa Ardhi Mteule wa Ofisi ya Ardhi Manispaa. |
| 16. | Simon Shoo | Kny ya Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi |
| 17. | Dr Elisha Robert | Mkuu wa Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe. |
| 18. | Richard Massawe | Mthibiti Ubora wa Shule. |
| 19. | Consolata James | Kny ya Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi |
| 20. | CPA Kishenyi Mulokozi | Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu |
| 21. | Rose Matunda | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria. |
| 22. | CPA Sunday Nkwambi | Mhasibu wa Mapato |

**D. WAALIKWA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Fabian Kamoga | - | Afisa Serikali za Mitaa |
| 2. | Ibrahim M. Makana | - | AAS MMI |
| 3. | Neema S. Rwegoshora | - | Kny: DAS |
| 4. | Insp Fatma Sato | - | DFO |
| 5. | Insp. Elizabeth Kaka | - | Uhamiaji |
| 6. | Evarst Kivuyo | - | Kny OCD |
| 7. | LT Col Ford J. Mwakasege | - | MJA |
| 8. | Jastin Nyatano | - | OCD |
| 9. | CPA. Eng. Andrew Kifua | - | Kny: RAS |
| 10. | Florence Fungawa | - | DSO |

11. Grace Massawe - DPO
12. Anold Makombe - M/Kiti CCM (W)
13. Naibu Katalambula - Katibu CCM (W)
14. Samwel Jackson - Katibu wa Mbunge

**E. WAKUU WA TAASISI**

1. Eng Daniel Ojwando - TEMESA
2. Nkinda Senni - RUWASA
3. Eng. Ibrahim Kiyungu - TANESCO
4. Eng Yohana William - TARURA
5. Eng Yusuph Katopola - SHUWASA

**F. WATENDAJI WA KATA**

1. Gaudiozi K. Mwombeki - Mtendaji wa Kata ya Ngokolo
2. Fortunatus L. Jilala - Mtendaji Kata ya Chamaguha
3. Elizabeth S. Mbate - Kny Mtendaji wa Kata ya Kolandoto
4. Adella Mukinga - Mtendaji wa Kata ya Kizumbi
5. Joshua Masengwa - Mtendaji wa Kata ya Ndala
6. Mwakaluba Jacob - Mtendaji wa Kata ya Old Shinyanga
7. Costantine M. Masalu - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Masekelo
8. Mahiba Pastory - Mtendaji wa Kata ya Lubaga
9. Abdul Kumalija - Mtendaji wa Kata ya Mwawaza
10. Simon Mashishanga - Mtendaji wa Kata ya Mjini
11. Patrick M. Dotto - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Ibinzamata
12. Mayala Ibrahim - Mtendaji wa Kata ya Kitangili
13. Michael Joshua - Mtendaji wa Kata ya Mwamalili
14. Sarah Wankuru - Mtendaji wa Kata ya Kambarage
15. Emilini Mtambu - Mtendaji wa Kata ya Ndembezi
16. Antony Charles - Kaimu Mtendaji wa Kata ya Ibadakuli
17. Ponsian Ngodita - Mtendaji wa Kata ya Chibe

**F: AFISA TARAFA**

1. Telezia K. Alois - Afisa Tarafa ya Mjini
2. Gregory Kachira - Afisa Tarafa ya Ibadakuli
3. Neema Mukandala - Afisa Tarafa ya Old Shinyanga

**G: WAANDISHI WA HABARI.**

1. Mwamvita Issa - Azam TV
2. Faustine Kasala - GOLD FM
3. Daniesa Malula - MALULA TV
4. Mapuli Misalaba - MISALABA MEDIA
5. Arnold Rukiza - SHY-MC

**SEKRETARIETI**

1. Esther Daudi — Mwandishi wa Vikao
2. Amina Juma — Mwandishi Mwendesha Ofisi

**Agenda za kikao zitakuwa kama ifuatavyo: -**

**Siku ya kwanza tarehe 29.04.2024**

1. Kufungua mkutano
2. Kuthibitisha agenda za mkutano.
3. Kupokea na kujadili taarifa za kwenye Kata kutoka kwa Madiwani wa Kata husika Pamoja na majibu ya changamoto za Kata kwa kipindi cha robo ya kwanza.
4. Kuahirisha kikao

**Siku ya pili tarehe 30.04.2024**

5. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani wa kawaida wa tarehe 30- 31.10.2023.
6. Kupokea Mihtasari ya Kamati za Kudumu kwa robo ya kwanza ya mwaka 2023/2024
    - Kamati ya Kudhibiti UKIMWI tarehe 13.01.2024
    - Kamati ya Mipango Miji na Mazingira wa tarehe 01.02.2024
    - Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu wa tarehe 02.02.2024
    - Kamati ya Fedha na Utawala wa tarehe 08.02.2024, 29.02.2024 na 22.02.2024.

7. Kupokea taarifa za utekelezaji wa Idara mbalimbali za kamati za kudumu kwa robo ya pili 2023/2024.
    - Kamati ya kudhibiti UKIMWI
    - Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu
    - Kamati ya Mipangomiji na Mazingira
    - Kamati ya Fedha na Utawala
8. Taarifa kutoka kwa Mkurugenzi kama zipo.
9. Masuala ya kiutumishi.
10. Kufunga kikao.

**AGD Na.01:2023/24** — **MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

**Kumb: BAR.03.1.1** — Mkutano wa Baraza la Madiwani wa kupitia taarifa ya robo ya tatu 2023/2024 Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe kuuliza maswali ya papo kwa papo kama ifuatavyo;

**Kumb: BAR.03.2.2** — **Swali:** Ni lini ghuba la kata ya Kolandoto Halmashauri ina mpango upi na kuzolewa taka katika ghuba hilo

**Jibu:** Ghuba hilo litafanyiwa kazi ila juhudi zinafanyika za matengenezo ya barabara ya kutokea Dampo ambapo ni tatizo la maeneo mengi ya Manispaa. Utatuzi ukikamilishwa uzoaji taka utaendelea katika eneo hilo na maeneo mengine. Hata hivyo Mkandarasi wa TARURA alishindwa kufikisha mitambo sababu ya hali ya mvua na ubovu wa Barabara. Aidha matengenezo yamefanyika kufukia na maeneo yenye shida Zaidi yanaendelea kutengenezwa.

**Kumb: BAR.03.2.3**

**Swali:** Halmashauri ina mpango upi kuhusu kutafuta mwekezaji wa kuanzisha kiwanda cha Sementi katika eneo la Mdau lililopo Kata ya Kizumbi

Ilielekezwa Menejimenti ilipokee suala hili na kulichakata kwa kina na kutoa ushauri kwa Waheshimiwa Madiwani.

**Kumb: BAR.03.2.4**

**Swali:** Halmashauri ilikuwa na mpango wa kuanzisha Stendi ya Magari katika Nguzo nane Mwawaza.
**Je?** Ni mpango upi uliopo wa kuanzishwa tendi hiyo ili kuepukana na ajali.

**Jibu:** Eneo lililokuwa machinga ya zamani mpango upo wa kuanzisha machinjio ya kuku na Stendi hiyo, Hivyo taratibu za awali zimeanza za tathimini kinachosubiriwa ni upatikanaji wa fedha.

**Kumb: BAR.03.2.5**

**Swali:** Halmashauri ina mpango gani wa kutengeneza kivuko katika Stend ya Ibinzamata.

**Jibu:** Mawasiliano yalifanyika na TANROAD ya kuweka kivuko na taa kwa akuwa kuna mpango pia wa kuanzisha gulio, hivyo mpango huo upo kwa ajili ya kurahisisha kuvuka kwa Wananchi

**Kumb: BAR.03.2.6**

**Swali:** Halmashauri ina mpango upi wa kuongeza ukubwa wa chumba na kitanda kingine katika Zahanati ya Chibe ili kurahisisha huduma ya kujifungua kwa wanawake.

**Jibu:** Utekelezaji utafanyika katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

**AGD Na.01:2023/24** **KUFUNGUA MKUTANO**

**Kumb: BAR.03.3.1**

Mwenyekiti alifungua Mkutano wa Baraza la Madiwani robo ya tatu saa 05.21 asubuhi kwa kuwakaribisha Wajumbe, Kamati ya ulinzi, Waandishi wa Habari na Wananchi katika Mkutano wa Baraza la Madiwani.

| | |
|---|---|
| **AGD Na.02: 2023/24** | **KUTHIBITISHA AGENDA ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 29- 30 .04. 2024.** |
| **Kumb: BAR .03.4.1** | Jumla ya agenda 10 zilithibitishwa kwenye Mkutano wa kawaida wa wa Baraza la Madiwani. |
| **AGD Na.03 :2023/24:** | **KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA KWENYE KATA KUTOKA KWA MADIWANI WA KATA HUSIKA.** |
| **Kumb: BAR.02.5.1** | Wajumbe waliwasilisha taarifa na changamoto za kila Kata na walielezea utatuzi wa Changamoto hizo na waliielekeza timu ya Menejimenti kutatua changamoto ambazo hazijapatiwa ufumbuzi moja kwa moja na kwa changamoto ambazo zinahitaji bajeti au utekelezaji wa muda mrefu Madiwani wapewe majibu. |

Wajumbe waliipongeza Menejimenti ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kwa jitihada zilizofanyika za kutatua changamoto katika Kata, hivyo kupelekea migogoro na hoja nyingi kupungua. Aidha, walitoa wito kwa timu ya Menejimenti kuendelea kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani katika kupunguza changamoto ili kuleta Maendeleo katika Manispaa ya Shinyanga.

Wajumbe walitoa hoja kuhusu suala la uendeshaji wa vikao vya kisheria kwa kuwa baadhi ya Watendaji hawafanyi vikao kwa mpangilio unaotakiwa.
Maelezo ya Ufafanuzi yalitolewa kuhusu uendeshaji/ufanyaji wa vikao vya Kisheria katika ngazi zote. Hata hivyo ilielezwa kuwa Ofisi ya Utumishi itafanya kikao na Watendaji wa Kata, Mitaa na Vijiji kuwaelekeza kufanya vikao vya kisheria kwa kufuata taratibu.

**Hoja kuhusu upungufu wa Watumishi/Wataalam katika ngazi za Kata**
Wajumbe walieleza kuwa katika baadhi ya Kata kuna upungufu wa Watumishi hali inayopelekea Wananchi kutopata huduma ipasavyo.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa upungufu wa Watumishi uliopo ni kwa nchi nzima hata hivyo mpango wa Ajira unaendelea kwa kuomba kibali cha kuajiri na utaratibu wa msawazo pia unafanyika.

Wajumbe walipokea maelezo ya ufafanuzi na ilielezwa kuwa suala la kupanga Watumishi lisimamiwe vizuri wapangwe kwa kuzingatia usawa hasa kwa upande wa walimu wa kike na wa kiume.

**Kumb: BAR.02.5.2** **Baada ya majadiliano Wajumbe walisisitiza Timu ya Menejimenti kufanyia kazi mambo yafuatayo;**

- Kusimamia usafi wa mazingira kwa kuwatumia wataalam katika ngazi ya Kata hususani Soko la Ndala.
- Walimu wa Shule za msingi na Sekondari wapangwe kwa uwiano kila shule wachanganywe walimu wa kike na wa kiume (Orodha ya walimu wa kike na wa kiume iwasilishwe kwa Mstahiki Meya)
- Kuwaelekeza Watendaji kufuata taratibu za uendeshaji wa vikao, kusoma taarifa za Mapato na Matumizi katika vikao vya kisheria.
- Kushughulikia posho za wenyeviti wa Mitaa
- Kuwaondoa wanawake wanaojiuza Kata ya Mjini Jirani na Ofisi ya Mtendaji.

**AGD Na.04 :2023/24:** **KUAHIRISHA KIKAO**

**Kumb: BAR.02.6.1** Kikao cha kujadili taarifa za Kata kiliahirishwa saa 07:27 mchana

**SIKU 2** **30.04.2024**

**AGD Na.06:2023/24:** **KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 15-16.02.2024.**

**Kumb: BAR.02.7.1** Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani wa tarehe 15-16. 02. 2024. ulisomwa ukurasa kwa ukurasa na wajumbe kuridhia kuwa yaliyomo ndiyo yaliyojadiliwa na hivyo ulithibitishwa na kuwa kumbukumbu halali wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kwa Mwenyekiti na Katibu kusaini Muhtasari huo.

**AGD Na.06:2023/24:** **KUPOKEA MIHTASARI YA KAMATI ZA KUDUMU YA ROBO YA TATU 2023/2024**

**Kumb: BAR.02.8.1** Kupokea Mihtasari ya Kamati za Kudumu kwa robo ya pili ya mwaka 2023/2024 ambayo tayari ilishathibitishwa katika vikao vya Kamati vilivyofanyika;

- Kamati ya Kudhibiti UKIMWI wa tarehe 31.01.2024
- Kamati ya Mipango Miji na Mazingira wa tarehe 01.02.2024
- Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu wa tarehe 02.02.2024
- Kamati ya Fedha na Utawala wa tarehe 08.02.2024, 29.02.2024 na 22.03.2024.

**Kumb: BAR.02.8. 2** Wajumbe waliipokea Mihtasari ya Kamati za kudumu na kuridhia kuwa kumbukumbu halali ya vikao vya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

| | |
|---|---|
| **AGD Na.07:2023/24:** | **KUPOKEA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA DIVISHENI MBALIMBALI ZA KAMATI ZA KUDUMU KWA ROBO YA TATU 2023/2024**. |
| **Kumb: BAR.02.9.1** | Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Divisheni na Vitengo mbalimbali vilivyo chini ya Kamati za Kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ambazo ni Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu, Kamati ya Mipango Miji na Mazingira, Kamati ya Kudhibiti UKIMWI, Kamati ya Fedha na Utawala kwa robo ya tatu 2023/2024 iliwasilishwa kwa Wajumbe.<br><br>Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili. |
| **Kumb: BAR.02.9.2** | Wajumbe walitoa hoja kuhusu fedha za Mbao zilizolipwa na Mzabuni Sh. 2,600,000/= ambazo hazikuletwa Shuleni na Mzabuni akaambiwa kurejesha fedha, ambapo zimerejeshwa imebaki Sh. 600,000/= Kamati ifuatilie ili fedha zilipwe zote. |
| **Kumb: BAR.02.9.2** | Ufafanuzi ulitolewa kuwa Fedha Sh 2,600,000/= Mzabuni alipewa barua ya kurejesha fedha zilizobaki Sh. 600,000/= na kufikia Mkutano mkutano wa baraza lijalo litafanyiwa kazi fedha zitarejeshwa.<br><br>Wajumbe walisisitiza ufuatiliaji ufanyike fedha hizo zirejeshwe |
| **Kumb: BAR.03.9.3** | Taarifa ya Mipango miji na Mazingira iliwasilishwa.<br>Taarifa ilipokelewa na kupitishwa |
| **Kumb: BAR.03.9.4** | **Taarifa ya Kamati ya Fedha na Utawala.**<br>Wajumbe walipongeza taarifa ya fedha za makusanyo katika mnada wa Old Shinyanga ambapo makusanyo hayo yamekusnywa na kuvuka lengo ikiwa ni pamoja na makusanyo ya machinjio ya Ndembezi**.**<br><br>**Hoja kuhusu Mapato ya Mradi wa Kiwanda cha uzalishaji wa Matofari kutokusanya mapato/kutofanya vizuri.**<br><br>Wajumbe walihitaji ufafanuzi kuhusu kusuasua kwa mradi wa kiwanda cha matofari cha Halmashauri.<br><br>Ufafanuzi ulitolewa kuwa mradi huu uzalishaji wake unasuasua kwa sababu taasisi zetu zinadaiwa ambazo ni Zahanati shule nk. Kamati |

ya Fedha imeelekeza taasisi zote zinazodaiwa zilipe fedha hizo ili kuinua mapato na kuongeza uzalishaji.
Aidha, kutokana na kusuasua kwa uendeshaji wa Kiwanda hicho Halmashauri imeamua kuanzisha kampuni itakayomilikiwa na Manispaa ya Shinyanga kwa jina la **SHINYANGA MUNICIPAL COUNCIL DEVELOPMENT COMPANY LIMITED**. Taratibu za usajili zimakamilishwa **tarehe 18.04.2024** kwa kupewa namba ya usajili **173956290 kampuni hii itatumika kuendesha miradi mbalimbali ikiwemo kiwanda hicho.**

**Hoja kuhusu mapato ya maegesho Stendi za Hiace katika Stendi zilizoanzishwa (Stend ya lubaga, Soko kuu, Kambarage, Nguzo nane).**
Wajumbe walihitaji ufafanuzi kuhusu namna ambavyo Halmashauri imeweka mkakati wa kukusanya mapato katika Stendi hizi.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Kamati ya fedha inaendelea kufanya ufuatiliaji pamoja na kuwa ushuru huo umerudishwa hivi karibuni kukusanywa na Halmashauri. utaratibu mzuri utawekwa wa namna ya kukusanya mapato hayo.

**Hoja kuhusu ufinyu wa eneo la mnada wa Old Shinyanga**
Wajumbe walieleza kuwa eneo linalotumika sasa kwa ajili ya shughuli za mnada halikidhi hivyo Mnada uhamishwe eneo la Butulwa kwa kuwa eneo hilo lilipwa fidia na kwa sasa halitumiki kwa shughuli yoyote.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Menejimenti itafanyia kazi ushauri huu pamoja na Kamati ya mipango miji ili kuona kama jambo hilo linawezekana la kuhamisha mnada kwenda katika eneo hilo.
Baada ya majadiliano wajumbe waliazimia kuwa;

**AZIMIO:**
Kuangalia uwezekano wa kuhamisha mnada wa Old Shinyanga kwenda Eneo la Butulwa.

**Hoja kuhusu makusanyo ya leseni za vileo kutokusanywa vizuri**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Leseni za vileo zimeanza kukusanywa mwezi wa nne mapato yataongezeka katika makusanyo ya robo ya nne 2024.

**Hoja kuhusu mapato ya vibali vya ujenzi**

Menejimenti iwatumie watendaji wa Kata kuhusu mapato ya vibali vya ujenzi kwa kuwatumia Watendaji ngazi ya kata na Mtaa na Mitaa kupata kanzi Data ili kukusanya kwa kutumia takwimu sahihi.

**Hoja kuhusu mapato ya madini ya ujenzi**

Wajumbe walipongeza juhudi za Menejimenti kwa makusanyo ya madini ya ujenzi walishauri kulipa fidia na kumiliki eneo ili mapato yawe ya Halmashauri**.**

**Hoja kuhusu mapato ya Ada ya Mabasi**

Wajumbe walitoa hoja kuhusu mabasi yanayokwepa kulipa ushuru huo, je ni utaratibu upi uliopo wa kukusanya mapato hayo ipasavyo.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Baada ya kuona baadhi ya mabasi yanakwepa kulipa ushuru, umewekwa utaratibu wa kukusanya mapato mchana na usiku ili kudhibiti upotevu wa mapato.

**Hoja kuhusu malipo ya posho za Wenyeviti wa Mitaa ambazo hazijalipwa.**

Wajumbe walieleza kuwa utaratibu ufanyike wa kuwalipa wenyeviti wa Mitaa posho ambazo hawajalipwa.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Manispaa ya Shinyanga imetenga Bajeti ya kulipa Wenyeviti wa Mitaa, kuwa kazi zao zinatambulika utaratibu wa malipo unaendelea na watalipwa fedha zao zote wanazodai Halmashauri.

**Hoja kuhusu kuanzisha mnada**

**Wajumbe walieleza kuwa Halmashauri iangalie umuhimu wa kujenga na kuanzisha mnada ili kuongeza mapato.**

Ufafanuzi ulitolewa kuwa Menejimenti inaendelea kulifanyia kazi na tayari miundombinu tayari imeanza kujengwa kwa ajili ya kuanzisha mnada Kata ya Ibadakuli (Mf. Choo nk)

**AGD Na.08:2023/24:** **TAARIFA KUTOKA KWA MKURUGENZI.**

**(i) Taarifa za Taasisi**

**(a) SHUWASA**

Ilielezwa kuwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Maningira Shinyanga (SHUWASA) imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali kuongeza mtandao wa majisafi katika maeneo ya Manispaa ya Shinyanga kupitia vyanzo mbalimbali vya fedha ikiwa ni pamoja na mapato ya ndani ya Mamlaka, Serikali Kuu na wafadhili. Aidha iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa kupitia mapato yake ya ndani Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa mazingira (SHUWASA), imetumia kiasi cha shilingi 81,983,290.20 kwa ajili ya kuongeza mtandao wa majisafi katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Shinyanga kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kata zinazonufaika na miradi hii ni pamoja na; Ibadakuli (Kilomita 1.37), Mwawaza (Mita 580), Kitangili (Kilomita 1.43), Kizumbi (Mita 996).

Ilielezwa kuwa Mamlaka ya majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) inaendelea na utekelezaji wa mradi mkubwa kupitia fedha za Mkopo wa riba nafuu toka shirika la Maendeleo la Ufaransa (French Development Agency; AFD) kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania. Mradi huu wenye thamani ya Euro milioni 76 (takribani Tsh. Bilioni 200) unahusisha kazi zifuatazo; -

i. Ujenzi wa mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 280
ii. Ukarabati wa mtandao chakavu wa majisafi unaofikia kilomita 100
iii. Ujenzi wa tangi mola la kuhifadhia maji lenye ujazo wa mita za ujazo 1,500 katika kata ya Kolandoto
iv. Ujenzi wa mitambo miwili ya kuchakata tope kinyesi (Ihapa, Mwagala);
v. Ukarabati mkubwa wa mtambo wa kutibu majisafi Ning'hwa na tathimini ya ufanisi wa bwawa la Ning'hwa na
vi. Ujenzi wa Jengo jipya la Ofisi.

Wajumbe walipongeza taasisi ta SHUWASA kwa huduma wanayoitoa ndani ya Manispaa ya Shinyanga na walihitaji kujua endapo maelezo yote yaliyotolewa kwenye kikao cha Kamati ya chama kama yametekelezwa.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa maelekezo yote yalipokelewa na yanaendelea kufanyiwa kazi, ilielezwa kuwa Magati yanachangamoto SHUWASA wanaendelea na utafiti kuhusu Mita za maji na endapo kama kuna magati yatahitajika ili wananchi wapate huduma itaangaliwa namna ya kufanya.

Mkurugenzi wa SHUWASA allipokea pongezi zilizotolewa na alieleza kuwa kikao alichoahidi kufanya na madiwani kitafanyika mwanzo wa mwezi June 2024. ambapo Waheshimiwa Madiwani watajadili masuala haya kwa kina zaidi.
Wajumbe waliipokea taarifa nakuipongeza taasisi hii kwa kwa kazi nzuri ya utoaji wa huduma katika Manispaa ya Shinyanga.

**(b) TARURA**

Taarifa ya utekelezaji wa miradi inayoendelea ya matengenezo ya Barabara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ina mtandao wa barabara wenye urefu wa 780.184, kilometa 193.635 ni barabara zinazounganisha kata na kata pia zinaunganisha tarafa na Wilaya Jirani (Collector Roads), Kilometa 585.549 ni barabara zinazounganisha kata na Kijiji (Feeder Roads). Aidha Halmashauri ina mtandao wa kilometa 22.562 za lami, kilometa 195.556 za changarawe na kilometa 562.466 za Udongo. Ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 TARURA Manispaa ya Shinyanga imetengewa jumla ya **Sh. 2,932,810,000.00** katika fedha hizi, fedha za matengenezo ya barabara ni Sh. **1,432,810,000.00,** fedha jimbo ni **Sh. 500,000,000.00** na fedha za tozo ya mafuta ni **Sh. 1,000,000,000.00**

Aidha hadi sasa taasisi imepokea jumla ya Sh. 586,654,350.00 sawa na **Asilimia 20%.** Ilielezwa kuwa, TARURA Manispaa ya Shinyanga inaendelea na utekelezaji wa miradi ya matengezo ya barabara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya miradi/Mikataba nane (08) ambayo ni asilimia ya utekelezaji ambapo katika miradi hiyo imegawanyika kama ifuatavyo; -

- Miradi mitano (05) ni fedha za mfuko wa barabara (Road fund) yenye thamani ya Sh. 1,003,280,653.25, ambayo inatekelezwa katika

baadhi ya Kata za Manispaa ya Shinyanga, miradi hiyo kwa sasa imefikia asilimia 76%. Aidha kuna miradi miwili (02) ya fedha za mfuko wa Barabara ambayo hado ipo kwenye mchakato wa manunuzi.

- Mradi mmoja (01) ni wa fedha za jimbo wenye thamani ya Sh. 475,000,000.00 ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia Asilimia 20% bado upo kwenye mchakato wa manunuzi
- Miradi miwili (02) ya fedha ya Tozo ya mafuta yenye thamani ya Sh. 597,227,440.00 miradi hiyo kwa sasa imefikia asilimia 18.5%. Aidha kuna mradi mmoja (01) wa fedha za Tozo za mafuta ambao bado ipo kwenye mchakato wa manunuzi.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa

Wajumbe waliipongeza TARURA kwa kazi wanazozifanya ndani ya Manispa ya Shinyanga ila waliomba yafanyike marekebisho eneo lililoharibika Barabara ya Mwawaza.

Ufafanuzi kuhusu hali ya barabara za Manispaa.
Matengenezo yanaendelea baada ya mvua kupungua ikiwa ni pamoja na matengenezo ya Madaraja kwa barabara zilizoharibika wakati wa mvua fedha za dharura zimeombwa kwa ajili ya matengenezo. Hata hivyo kuanzia tarehe 2 TARURA watapita kila Kata ili kufanya mapitio ya bajeti.

**AGD Na.08:2023/24:** **TAARIFA ZA MKURUGENZI**

Taarifa ya majenzi yanayoendelea kutekelezwa ambayo ni jengo la Utawala, Nyumba ya Mkurugenzi, Nyumba ya Mkuu wa Divisheni, ujenzi wa vibanda Soko Kuu upande wa juu na bwalo la Chakula Shule ya Wasichana Shinyanga ilitolewa kwa wajumbe.

**Kumb: BAR.02.10.5** Ilielezwa kuwa Halmashauri Kupokea wageni watakaotekeleza mradi wa TACTIC ambao watajenga Soko, Stend na wameombwa kujenga roli parking na carwash. taratibu zikikamilishwa wajumbe wataendelea kufahamishwa kila hatua.

Aidha Utengenezaji wa Madawati unaendelea na kwa kuwa ni zoezi endelevu madawati yataendelea kutengenezwa hadi Desemba, 2024.

Mwisho alitoa shukrani kwa ushirikiano unaotolewa na Waheshimiwa Madiwani katika shughuli zote za kuleta maendeleo katika Manispaa ya Shinyanga.

**AGD Na.09:2023/24:** **KUFUNGA MKUTANO**

**NASAHA ZA VIONGOZI**

**Kaimu RAS**

- Halmashauri kutenga fedha za mafunzo ya wenyeviti wa Mitaa/Vijiji na Vitongoji, ushauri kuendelea kutenga 90% ya fedha za wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.
- Matumizi ya fedha za Halmashauri yaendane na bajeti na vifungu vilivyokasimiwa.
- Kupongeza Halmashauri kupata hati safi.
- Kuanzisha Vituo vya polisi kwenye Kata

**Katibu CCM Wilaya**

- Kupongeza Baraza la Madiwani kwa kazi kubwa wanayoifanya, pia kusisitiza kufanyika semina ya Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji.
- Kushukuru utulivu ndani ya Baraza hivyo ushirikiano uendelee.

**Mstahiki Meya**

- Wataalam kupitia vema BOQ wakati wa utekelezaji wa miradi ili fedha zinazoletwa kutoka Serikali zikamilishe mradi husika bila kuongeza fedha za mapato ya ndani.
- Waheshimiwa kufuata taratibu za kuchangia hoja katika vikao kwa kuchangia hoja zilizopo mezani.
- Kuhamisha wafanyabiashara eneo la Mtaa wa Sukari.

**Kumb: BAR.02.12.1** Mwenyekiti alifunga Mkutano saa 7:52 mchana kwa kuwashukuru Wajumbe, waalikwa, Waandishi wa Habari, Wananchi pamoja na Wataalam kwa kushiriki vizuri Mkutano wa Baraza la Madiwani.

**KUMBUKUMBU HIZI ZIMETHIBITISHWA NA**

| | |
|---|---|
| _________________________ | _________________________ |
| Mwl Alexius R. Kagunze | Mhe. Elias R. Masumbuko |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

**TAREHE**________________